**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Uturuki**

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Alhamisi, 9 Shawwal 1445 H | 18/04/2024 M | Na: 1445 / 12

## Taarifa kwa Vyombo vya Habari

### Hizb ut Tahrir / Wilayah Uturuki
### Yatangaza Kufariki kwa Mmoja wa Dada Mwema Sükîna Aslan

(Imetafsiriwa)

Sükîna Aslan, ambaye alikuwa miongoni mwa kina dada wa kwanza nchini Uturuki ambaye alibeba da'wah na kujitolea maisha yake kuregesha maisha kamili ya Kiislamu kama mwanamke mwema na muumini, alisalimisha roho yake jana kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema.

[إنّا لله وإنّا إليهِ رَاجعُون]

**"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea."** [Surat Al-Baqara:156]

Sükîna alikuwa akipokea matibabu ya ugonjwa mkali kwa miaka 17. Tunashuhudia kwamba alivumilia ugonjwa wake na dhiki zake kwa subira, na alikuwa mwanamke aliyejitolea katika kazi yake ya da'wah na kwa familia yake. Tunaomba kwamba dada yetu mpendwa aweze kufinikwa katika rehma pana ya Mwenyezi Mungu na kwamba familia yake ipate subira. Tunatoa rambirambi zetu kwa jamaa zake, wapendwa, na kina dada katika da'wah. Mwenyezi Mungu aifanye mitihani aliyovumilia iwe kafara kwa dhambi zake na kumlipa kwa pepo.

[إِنَّمَا يُوَفَّى الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ]

**"Hakika wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu."** [Surat Az-Zumar:10]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Uturuki**